# Jamii ya wafugaji yakumbukwa

Aurea Simtowe, Mwananchi
asimtowe@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Nzunda amesema kuwa Jamii inayojishughulisha na shughuli za ufugaji haijanufaika kikamilifu licha ya jitihada zinazofanywa katika sekta hiyo.

Nzunda alisema hayo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa wadau wa maendeleo ya sekta ya mifugo kutoka taasisi za Serikali na sekta binafsi.

Mkutano huo pia ulijadili Mpango wa mabadiliko ya sekta ya mifugo kwa miaka mitano ijayo kwa mwaka 2022/2023 hadi 2026/2027.

Nzunda alisema wadau wengi waliopo kwenye sekta ya mifugo hawana mipango jumuishi inayogusa jamii hiyo, hivyo alitoa rai kwa wadau hao kuhakikisha mipango yao inagusa moja kwa moja shughuli za wafugaji.

"Wafugaji wengi wanalalamika kuwa wadau wanaojihusisha na sekta yao wanatumia rasilimali nyingi kwenye maeneo yasiyogusa moja kwa moja maslahi yao," alisema Nzunda

Alitumia nafasi hiyo kuyashukuru mashirika ya kimataifa na taasisi zisizo za kiserikali ambazo zimejielekeza kutatua changamoto za wafugaji moja kwa moja na mengine yamejikita kwenye tasnia za maziwa, malisho na kuboresha mbari za wanyama.

Aliwataka wadau wanaokwamishwa na vikwazo mbalimbali kwenye jitihada zao za kutaka kuendeleza sekta ya mifugo wafike ofisini kwake ili wasaidiwe kutatua vikwazo vinavyowakabili. "Upo usemi unaosema ukitaka kufika haraka tembea mwenyewe na ukitaka kufika mbali tembea na wenzio hivyo na sisi kama Serikali tupo tayari kutembea pamoja na wadau wote wa sekta ya mifugo ili tufike mbali," alisema Nzunda.

**2022/23**

**Mwaka ambao mpango huo umeanza.**

**2026/27**

**Mwaka ambao mpango huo wa mabadiliko ya sekta ya mifugo.**

Akiwasilisha mpango huo, Kaimu Mkurugenzi wa Sera na Mipango (Mifugo), Mbaraka Stambuli alisema kuwa lengo kuu la mpango huo ni kuimarisha sekta ya mifugo ili kuiwezesha kuwa na tija, kuchangia uchumi wa viwanda, kuimarisha biashara ya ndani na nje ya nchi na kunufaisha wananchi kwa ujumla.

"Utekelezaji wa mpango huu una maeneo saba ya kimkakati ambayo yatatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2022/2023-2026/27) na miongoni mwa maeneo hayo ni kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, kuimarisha huduma za maji, malisho, vyakula vya mifugo na kuboresha huduma za ugani," alisema Stambuli.

Kwa upande wa Elinman Lyatuu, mmoja wa wadau walioshiriki mkutano huo ambaye ni mwakilishi kutoka Taasisi ya kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) alisema taasisi yao ipo tayari kuunga mkono jitihada za Serikali hasa kwenye eneo la utambuzi wa idadi ya mifugo kutumia mifumo ya Tehama na eneo la uboreshaji teknolojia ya uhimilishaji.

"Natambua kupitia mpango huu itatengenezwa kanzidata ambayo itatumika kufanya tathmini za shughuli mbalimbali za ufugaji hapa nchini, hivyo nashauri kanzidata hiyo iwe kwenye lugha rahisi ambayo wafugaji wataielewa kwa urahisi," alisema Lyatuu.

Zaidi ya Sh1.9 bilioni zinatarajiwa kutumika kutekeleza jumla ya maeneo saba ya kimkakati yaliyopo kwenye mpango huo wa miaka mitano ambao unatarajiwa kuwa suluhu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta

Scanned with CamScanner

MZALENDO UK 13

# Wafugaji watakiwa kutambua umuhimu kuvisha mifuko hereni

**Na HAPPINESS MTWEVE,** *Dodoma*

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wafugaji kutambua utaratibu wa kuvisha hereni mifugo si hiari, bali ni lazima lengo likiwa ni kukuza soko la mifugo ndani na nje ya nchi ikiwemo kufuga kwa tija.

Pia, amezitaka halmashauri na wafugaji, kuchukua tahadhari kutokana na matarajio ya uwepo wa uhaba wa malisho kulingana na mabadiliko ya tabia nchi ili wasipoteze mifugo kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Alitoa kauli hiyo jijini hapa jana wakati akifungua Mkutano Maalumu wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), ulioenda pamoja na uzinduzi wa uvishaji hereni mifugo.

Ndaki alisema kwamba, wafugaji wanapaswa kuzingatia suala la uvishaji hereni katika mifugo yote, badala ya kuweka chapa ili kuendana na soko la dunia.

Alisema wafugaji wakifanya hivyo, itawasaidia kutambua mifugo yao, hata ikipotea kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa sababu watakuwa na hereni ambazo ni utambulisho wa mifugo kutoka eneo fulani.

Alisema baada ya uzinduzi wa uvishwaji hereni, wafugaji wanapaswa kuwa tayari kuvisha hereni katika mifugo na kuondokana na dhana ya kupiga chapa wanyama ikiwemo kufuga kwa mazoea.

Kuhusu tahadhari ya uwepo wa uhaba wa malisho kwa mifugo, alisema halmashauri na wafugaji, wanapaswa kuchukua tahadhari kwa kurasimisha maeneo waliyonayo ambayo yatawasaidia kuandaa mashamba ambayo watahifadhi malisho.

Alisema wafugaji kuhifadhi malisho ni jambo muhimu kwa sababu, kipindi cha kiangazi kunakuwa na uhaba wa malisho na kusababisha migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Alisema maeneo ambayo yametengwa ni ya wafugaji lazima yarasimishwe ili yajulikane, jambo ambalo litachangia kupunguza migogoro kwa wafugaji, ikitokea yamevamiwa ni rahisi serikali kuingilia kati.

Kuhusu suala la uchimbaji malambo ya maji kwa ajili ya mifugo, alisema kuna vifaa vitaletwa ambavyo vitasaidia kuchimba malambo katika maeneo ya wafugaji ili kuhakikisha mifugo haikosi maji.

Hivyo, aliwataka wafugaji kupeleka mapendekezo, kwa sababu Wizara inapitia upya sera ya mifugo na sheria ili wafuge kwa tija na kibiashara.

**WAFUGAJI**

**UTARATIBU**

Alisema maeneo ambayo yametengwa ni ya wafugaji lazima yarasimishwe ili yajulikane.

Scanned with CamScanner